Mawasiliano

# JE, UINJILISTI NI NINI HASA?

Mwandishi Ndugu Gerhard

Si swali la ajabu hilo!  Kila Mkristo anajua Uinjilisti ni nini!  Kweli?

Neno hilo 'uinjilisti' asili yake ni neno la Kiyunani 'euangelion' lenye sehemu mbili: 'eu' = 'njema', na 'angelos' = ujumbe.  Katika Biblia tunakuta neno hili limetumika mara 78, likitafsiriwa mara nyingine 'injli' na mara nyingine 'habari njema'.

Mara chache pia neno hilo limetafsiriwa 'mahubiri', lakini neno halisi la Kiyunani lenye maana ya 'kuhubiri' ni 'kerusso', linalopatikana mara 52 katika Agano Jipya. Linaweza pia kutafsiriwa 'kutangaza'.

Wazo lenyewe ni hilo:  Mfalme huwatuma wapiga mbiu wake watangaze ujumbe kwa watu wake.  Wanatakiwa waende kila mahali wakitangaza tu ujumbe huo. Hawaulizi maoni ya wale watu, wala kuwashawishi wakubali ujumbe huo au kuujadili. Wanautangaza tu.  Watu wanatakiwa kusikiliza kwa makini na kutenda kufuatana na ujumbe huo. Lakini wanaweza kufanya hivyo hapo tu ambapo wameuelewa kikamilifu.  Mtu yeyote hawezi kulaumiwa kwa kutokutii maagizo ya mfalme ikiwa yule mpiga mbiu ameubadilisha au kuufupisha ujumbe ule, au kutumia lugha ambayo wale watu hawawezi kuifahamu.

Na ndicho kiini cha somo hili.  Kila Mkristo ni mwinjlisti, yaani mjumbe aletaye habari njema. Siyo tu ndani ya jengo la kanisa au katika mkutano wa kiroho wa kuhubiri, bali pia katika kuwashirikisha watu wanaotuzunguka.

Ni muhimu sana tujifunze kuongea kwa njia inayowawezesha wenzetu waelewe yale tunayotaka kuwaambia, au tuseme kwa usahihi zaidi, yale ambayo Mungu anataka kuwaambia.  Tatizo letu mara nyingi siku hizi ni kwamba Wakristo wanafikiria kwa makini zaidi mbinu za kufanya uinjilisti, kuliko kutafakari ujumbe wenyewe wa Injili.  Mikutano mikubwa na kampeni za kuhubiri na kuponya hufanywa na 'wahubiri wenye nguvu', vikundi vya muziki na waimbaji. Inaonekana kwamba watu wengi wanafikiri njia bora ni ile inayotumia muda mfupi na kutendeka kwa urahisi. Tumezoea kurahisisha Injili kwa kukaza umuhimu wa kumpokea Kristo kama Mwokozi, hata tunasahau kueleza kwa nini inampasa mtu afanye hivyo.

Lakini ni muhimu kabisa, hasa tunapowasiliana na Mwislamu, ambaye anafikiri na kufahamu kwa njia tofauti sana na yetu. Maneno tuliyoyazoea (kama "lazima ufike chini ya Msalaba"), na ya kidini mengine (kama "kuokolewa kwa neema", "kuzaliwa mara ya pili" "kujazwa na Roho") yanakuwa kinga badala ya daraja katika kuwasiliana na Mwislamu wa kawaida kuhusu Injili.

Inatupasa tufahamu kwamba Mwislamu anaelewa mambo ya kiroho tofauti kabisa na sisi. Yeye huamini kwamba mwanadamu kimsingi ni mwema, kwa hakika ni mwema kutosha kustahili kuokolewa kama atatimiza masharti ya kidini kama impasavyo. Hebu tafakari maneno haya ya mwalimu mmoja wa Kiislamu: "Kufuatana na maoni ya Kiislamu wanadamu hawakuanguka wala kuokolewa. Kwa sababu hawajaanguka, hawajahitaji mwokozi. Lakini pia, kwa sababu hawakuokolewa, inawapasa watende mambo mema... Ni sifa na utukufu wao kujiokoa kwa njia ya matendo yao."1 Kwa hiyo Mwislamu haelewi kabisa uzito wa dhambi, hivyo haoni haja ya ukweli wa ki-Biblia kwamba Mungu katika Kristo alitupatanisha naye kwa kukubali kuvumilia pale Msalabani adhabu ambayo sisi tulistahili kupitia. "Mshahara wa dhambi ni mauti", (Warumi 6:23), kwa hiyo Kristo alifanywa ile "adhabu ya kifo" badala yetu.

Kwa hiyo tunaweza kutazamia kwamba karibu kila Mwislamu ana maoni juu ya Mungu, binadamu, sheria ya Mungu, dhambi na haja ya kupatanishwa na Mungu, ambayo si ya ki-Biblia. Ni kweli kwamba Waislamu pia hutumia maneno yanayopatikana katika Biblia, kama vile sala, dhambi, msamaha, dhabihu, neema, toba, mbingu na jehanum, Ibrahimu, Musa, Yesu na mengine; lakini kwa mawazo yake Mwislamu, maana ya maneno hayo ni tofauti kabisa na maana yake kwa mawazo ya Mkristo.

Tukilinganisha mambo hayo yote, tunaona kwamba kazi ya "kuwahubiri Habari Njema" Waislamu si rahisi. Inatubidi tuainishe, kufafanua na kutoa mifano hai kuhusu mambo tunayotaka kuwasilisha. Kabla hajaweza kukubali kuwa Mkristo, mwanamume au mwanamke Mwislamu hana budi aelewe kinaganaga kweli za msingi kabisa kuhusu Mungu, binadamu, dhambi, sheria ya Mungu na neema Yake. Kushirikisha Injili ni kuwafahamisha mambo yafuatayo:

**Mungu ni Nani?** Hatuwezi kumwona wala kumsikia. Kwa hiyo watu wengi wamebuni akilini mwao mfano wanaofikiri ni wa 'mungu' wao. Lakini Mungu amejifunua kwetu katika Neno Lake, ili tujue yote juu Yake ambayo akili zetu dhaifu zinaweza kutambua. Mungu ni mtakatifu na mwenye haki, naye "amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa" (I Timotheo 6:16). Kwa sababu ya utakatifu Wake hawezi kushirikiana na mwanadamu mwenye dhambi, kama vile moto hauwezi kushikamana na maji.

**Binadamu ni nani?** Bila shaka tunajua jibu la swali hili vizuri zaidi. Sisi ni wanadamu, kwa hiyo inatupasa tujifahamu. Lakini tunajuaje? Tunajilinganisha na watu wengine na kufikiri kwamba sisi ni wema au kwa vyovyote sisi si wabaya kuliko wengine walio wengi. Lakini Mungu hampimi mwanadamu kwa mlingano huo. Anatulinganisha na Yeye Mwenyewe. Naye alifikia uamuzi huu: Binadamu ni mwovu "na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya sikuzote" (Mwanzo 6:5)! Kwa hiyo,, Mungu asipofanya tendo maalum la kutubadilisha,

hatuna tumaini lolote, kwa sababu hatuwezi kujibadilisha sisi wenyewe, wala kufuta maovu yetu tuliyokwisha kuyatenda.

**Sheria ya Mungu** hutupatia kipimo cha Mungu cha kujilinganisha nacho na kusawazisha uhusiano wetu na Yeye na kati yetu sisi wenyewe. Sheria hiyo hutufunulia jinsi tulivyoanguka kabisa, lakini pia hutuonyesha njia ya kutoka katika hali hiyo: dhabihu ya kuteseka na kufa badala yetu.

**Kuvunja Sheria ya Mungu** pamoja na uovu wote na ukosefu wa imani kwa Mungu ni dhambi: "Maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone" (Isaya 59:2). Hata njia zetu za kuwaza ni mbovu na zenye makosa. Kwa hiyo kila mwanadamu anatengwa na Mungu. Na dhambi iliyo mbaya kuliko nyingine zote ni kwamba mwanadamu anafikiri anaweza kurekebisha hali yake hiyo kwa njia ya matendo mema ya kidini ya kumpendeza Mungu. Ni hapo tu ambapo mtu ametambua hayo yote, ndipo amefikia mahali pa kuweza kukubali ujumbe wa Habari Njema.

**Neema ya Mungu** hufunuliwa kwetu "kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi". (Warumi 5:8) "Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao.." (II Wakorintho 5:18+19). Uinjilisti ni kuwasilisha na kushirikisha ukweli huo kwa njia zinazoeleweka kikamilifu akilini mwa jirani zetu.

*I Petro 3:14b,15 hutupatia mwongozo mzuri sana kwa uinjilisti: "Mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu! Mwe tayari sikuzote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu."*
Hebu tafakari mambo hayo basi!

1. "Uislamu", mwandishi Isma'il R. Al Faruqi, uk.9.